

MUHTASARI WA TAARIFA YA HUDUMA ZA AFYA MKOANI SINGIDA

28/09/2016

1.1 VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Mkoa wa Singida una jumla ya vituo 221 vya kutolea huduma za Afya ikiwa ni:

	Serikali	Mashirika	FBO/NGO	Binafsi
Hospitali - 9	3	0	6	0
Vituo vya Afya - 17	15	0	1	1
Zahanati - 195.	167	0	20	8
Jumla	185	0	27	9

- Sera ya Afya ya mwaka 2007 katika mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wenyе lengo la kuimarisha na kusogeza huduma za Afya karibu na wananchi kwa kuhakikisha kwamba kila Mkoa unatakiwa kuwa na:
 - Hospitali ya Rufaa,
 - hospitali ya Wilaya,
 - kila Kata kuwa na kituo cha Afya na
 - kila kijiji kuwa na Zahanati kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma hii,
- Aidha Halmashauri zinatakiwa kuendelea kuwahamasisha wananchi kuibua miradi ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati katika maeneo mbayo hayana vituo hivyo.

Jedwali hapo chini linaonesha kuwa Halmashauri mbili tu (Iramba na Manyoni) ndizo zenyé idadi kubwa ya Zahanati yaani zaidi ya 50%.

Halimashauri	Idadi ya watu	Vituo vya Afya					Zahanati			
		Idadi ya Kata	Vilivyopo	%	Upungufu	Idadi ya Vijiji/ Mtaa	Zilizopo	%	Upungufu	
Iramba DC	261370	20	3	15	17	70	37	53	33	
Manyoni DC	216376	19	2	11	17	58	33	57	25	
Ikungi DC	301941	28	3	11	25	101	34	34	67	
Mkalama DC	208772	17	4	24	13	70	29	41	41	
Singida DC	249466	21	2	10	19	84	28	33	56	
Singida MC	166346	18	2	11	16	72	17	24	55	
Itigi DC	111896	11	1	9	10	41	17	41	24	
Total	1,516,167	134	17	13	117 (87%)	496	195	39	301 (61%)	

Vituo vinavyoendelea kujengwa

- Kuna jumla ya vituo vya kutolea huduma za Afya 69 vinaendelea kujengwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Singida

Jina la Halimashauri	Idadi ya Hospitali	Idadi Vituo vya Afya	Idadi ya Zahanati	Jumla
Singida MC	-	-	1	1
Singida DC	-	3	11	14
Iramba DC	-	6	11	17
Manyoni DC	-	2	4	6
Ikungi DC	-	2	11	13
Mkalama DC	-	7	9	16
Itigi DC	-	2	0	2
Jumla	-	22	47	69

- Kukamilika kwa vituo hivi kutaongeza vituo vya kutolea huduma za Afya kutoka 221 hadi 290, hivyo kuwa na upungufu wa Zahanati 254(52%) na vituo vya Afya 95(78%).
- Aidha halmashauri zinatakiwa kuwa na mikakati endelevu ya kukamilisha ujenzi wa Vituo na Zahanati ambayo miradi yake imeibuliwa na wananchi.

Ngazi ya Mkoa

- Timu ya usimamizi wa shughuli za Afya ya Mkoa itafanya uhamasishaji wa ukamilishaji wa angalau kituo kimoja katika kila halmashauri.
- Kila halmashauri iainishe kituo kimoja kinachotakiwa kufanyiwa uhamasishaji ili zoezi hilo lifanyike mara moja.

NYUMBA ZA WATUMISHI

Nyumba za watumishi ni moja ya mahitaji muhimu kwa Watumishi wa Afya hasa wanaofanya kazi maeneo ya vijijini ambako miundombinu ya upatikanaji wa huduma ni hafifu. Mkoa una jumla ya nyumba za

Jina la Halimashauri	Mahitaji	Zilizopo	%	Upungufu	%
Singida MC	57	18	32%	39	68%
Singida DC	173	63	36%	110	64%
Iramba DC	160	82	51%	78	49%
Manyoni DC	272	56	21%	226	83%
Ikungi DC	146	69	47%	77	53%
Mkalama DC	104	39	38%	65	63%
Itigi DC	160	18	11%	142	89%
Jumla	1,072	345	32%	737	69%

- Halmashauri ya Iramba ina idadi kubwa ya nyumba za watumishi ukilinganisha na Halmashauri nyingine.
- Hata hivyo uwepo wa nyumba za watumishi unaongeza chachu na motisha katika utendaji kazi kwa kuzingatia ikama ya sasa inayohitaji watumishi 9 hadi 15 katika ngazi ya Zahanati na 35 hadi 45 katika vituo vya afya.

Changamoto zinazokabili eneo la Vituo vya Kutolea huduma za Afya

- ▶ Mkoa unakabiliwa na upungufu mkubwa wa vituo vya kutolea huduma za Afya kwani kuna upungufu wa Zahanati 301 Vituo vya Afya 134 na Hospitali za Wilaya 5 (Ikungi, Singida DC, Mkalama na Itigi, Singida MC). Hata hivyo kwa halmashauri za Ikungi na Singida DC wanatumia hospitali za Makiungu na Mtinko kama DDH.
 - Mtinko – Mkataba haujakamilika na mazungumzo yanaendelea
 - Iambi hakuna makubalianO/mazungumzo yaliyoanzishwa
- ▶ Baadhi ya Vituo vya Afya na Zahanati havijafanyiwa ukarabati kwa kipindi kirefu (mfano kituo cha Afya Itigi).
- ▶ Kutotolewa kwa fedha za MMAM kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo kunakwamisha mwitikio wa Wananchi kuendelea kuchangia ujenzi wa vituo kwa kujenga maboma ya vituo na kufanya baadhi ya vituo kukaa kwa kipindi kirefu bila ujenzi kukamilika. Hata hivyo hili ni jukumu letu sote tulipo hapo.

UBIA BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI

- Aina za huduma zinazopatikana kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.
 - Uhamasishaji wa afya bora (Promotive services), Kinga (preventive services), Tiba (Curative services), Utengamao (Rehabilitative services) Tiba shufaa (Palliative care).
- Tumekuwa na ushirikiano wa karibu na mzuri kati ya vituo binafsi na wasimamizi wa huduma za afya na Kuweza kupeleka huduma za afya pale ambapo huduma hazipatikani.

CHANGAMOTO

- Watumishi wasiokidhi Vigezo wanaendelea kutoa huduma za afya.
- Wamiliki kufungua vituo bila kufuata utaratibu na kutoa huduma bila kuwa na kibali. mfano maduka ya dawa muhimu, maabara za afya, zahanati n.k
- Kutokuwepo kwa mfumo mmoja wa utoaji huduma unaoshirikisha wadau wote (mfano mfumo wa rufaa – “Vertical and Horizontal referrals”)

1.2 HALI YA WATUMISHI WA AFYA KATIKA MKOA

- Mkoa una jumla ya Watumishi 1,804 wa kada mbalimbali za afya kati ya 4,238 wanaohitajika; kuna upungufu wa Watumishi 2,404 sawa na 57% ya mahitaji.
- Upungufu Mkubwa upo katika kada za Madaktari, Matabibu, Wauguzi na Watekinolojia wa Maabara na Dawa.

Hali ya watumishi wa afya katika Mkoa (walioajiriwa na Serikali)

Jina la Taasisi	Mahitaji	Waliopo	%	Upungufu	%
RHMT	8	7	88%	1	13%
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa	682	378	55%	302	44%
Singida MC	438	170	39%	268	61%
Singida DC	672	313	47%	359	53%
Manyoni DC	639	265	41%	346	54%
Iramba DC	623	265	43%	358	57%
Ikungu DC	381	120	31%	261	69%
Mkalama DC	447	221	49%	226	51%
Itigi DC	348	65	19%	283	81%
Jumla Mkoa	4,238	1,804	43%	2,404	57%

Hali ya watumishi wa afya...cont

- Vituo vya kutolea huduma za Afya visivyokuwa vya Serikali vina mchango mkubwa katika kuboresha utoaji huduma kwa maeneo mbalimbali katika mkoa huu.
- Vituo hivi pia vinakabiliwa na upungufu wa watumishi kama ilivyo kwa vituo vilivyo chini ya Serikali.

Hali ya watumishi wa afya katika Mkoa (walioajiriwa Katika Mashirika ya Dini)

Jina la Taasisi	Mahitaji	Waliopo	%	Upungufu	%
Hospitali ya Rufaa ya Mt Gasper-Itigi	438	203	46%	235	54%
Makiungu CDH	357	164	46%	193	54%
St Carolous- Mtinko Hospit	200	107	54%	93	47%
Iambi Hospit	310	127	41%	183	59%
Kilimatinde Hospit	98	39	40%	59	60%
Malikia wa Ulimwengu (Puma) Hospit	312	62	19.4%	252	81%
Jumla Mkoa	1,715	702	41%	1,015	59%

MCHANGO WA SERIKALI KATIKA HOSPITALI ZA MASHIRIKA YA DINI TSHs. 3,243,109,948

Aina ya Mchango inayotoa serikali	Makiungu CDH	St Gasper Hospital	St Carouus Mtinko	Iambi Hosp	Kilimatinde Hosp
Staff Mishahara Mwaka)	Grants(kwa	497,919,600	657,246,000	343,944,000	397,896,000
Mishahara watumishi serikali attached FBOs mwaka)	ya wa walio kwenye kwa	173,088,000	66,720,000	133,872,000	108,756,000
Basket zinazotolewa mwaka	Fund kwa	196,493,250	33,566,380	33,341,700	30,000,000
Budget ya dawa msd		82,181,722	167,294,076	0	0
Fedha nyinginezo zinazotolewa mwaka	kwa	17,849,000	0	9,957,000	0
Jumla		967,531,572	924,826,456	521,114,700	292,985,1220

Changamoto zinazokabili eneo la watumishi katika Sekta ya Afya

- ▶ Kutokuwepo kwa mipango endelevu ya “**Retention scheme**” ya Watumishi” katika Sekta ya afya
- ▶ Uhaba wa nyumba za Watumishi
- ▶ Muongozo wa Uandaaji wa makisio ya bajeti ya Mishahara ya Watumishi usiozingatia Ikama ya Watumishi katika Sekta ya Afya
- ▶ Upangaji mbovu/mbaya wa Watumishi katika vituo usiozingatia uzito wa kazi na majukumu kwa kila kituo. Mfano Zahanati ya Puma katika halmashauri ya Ikungi ina Matabibu wawili huku Zahanati ya Mgungila inayoona wagonjwa wengi kuliko Puma ikiwa haina Tabibu hata mmoja.

1.3 HALI YA UPATIKANAJI WA DAWA, VITENDANISHI NA VIFAA TIBA KATIKA MKOA

- ▶ Kwa kipindi cha Julai 2015 mpaka sasa, hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyakutolea huduma ni ya kuridhisha.
- ▶ Aidha kwa dawa muhimu (tracer medicines) Wastani vituo vina 80% dawa hizo.
- ▶ Hii inamaanisha katika bidhaa muhimu 30 (tracer medicines) vituo vina upungufu kati ya aina 4-6 ambazo mara nyingi zinakuwa ni antibiotics na vifaa, ambazo hukosekana mara kwa mara katika vituo vyakutolea huduma za afya.

Changamoto zinazolikabili eneo la dawa Mkoani Singida.....

- Uhaba wa baadhi ya dawa na vifaa tiba katika vituo vyakutolea huduma za afya.
- Maombi ya dharura ya mara kwa mara ya dawa na vifaa tiba
- Mrundikano wa baadhi ya dawa katika stoo za vituo inayopelekea kuongezeka kwa dawa zinazoisha muda wa matumizi kabla hazijatumika.
- Upotevu wa dawa usiokuwa na maelezo ya kuridhisha.

Sababu zinazopelekea changamoto zinazolikabili
eneo la dawa mkoani Singida.....

- ❑ Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za manunuzi ya dawa na vifaa tiba kupitia MSD.
- ❑ Baadhi ya Halmashauri kutotumia fedha za CHF/NHIF katika manunuzi ya dawa **kama miongozo inavyoelekeza.**
- ❑ Kuchelewa kupata fedha za Mfuko wa pamoja (Health Basket Fund).
- ❑ Matumizi hafifu ya fedha za bakaa Katika Robo ya kwanza kila mwaka wa fedha.


Sababu zinazopelekea changamoto zinazolikabili eneo la dawa Mkoani Singida.....

- ❑ Usimamizi hafifu wa matumizi sahihi ya dawa/ Vipimo Katika vituo vya kutolea huduma za afya hasa vituo binafsi.
- ❑ Vituo vingi kutoingiza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba kwenye vitendea kazi mbalimbali. Mfano leja ya mali, fomu za kutolea dawa kwa wagonjwa (prescription forms), rejesta mbalimbali.....
- ❑ Uhamasishaji mdogo katika Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) na NHIF ambapo mpaka sasa Hakuna Halmashauri iliyofika 50% ya kaya zilizojiiunga na CHF.
- ❑ Uhaba wa wataalam wa dawa Katika Vituo vya kutolea huduma.

Sababu zinazopelekea changamoto zinazolikabili
eneo la dawa mkoani Singida.....

- ❑ Kutofanya kazi kwa timu za kitaalam (Council technical committees and Therapeutic committees).
- ❑ Kutoza kiwango cha chini (5,000) kwa kaya moja ya watu 6 manispaa ya singida wakati utaratibu ni TIBU kwa KADI (TIKA) Ambapo ghamama yake ni Tshs. 10,000/= kwa mtu 1.
- ❑ Usimamizi hafifu wa maeneo ya kutolea huduma za afya hasa maduka ya dawa ya vijijini ambayo huendeshwa na watu wasio na sifa.

MATOKEO YA UHAKIKI WA MATUMIZI YA DAWA KATIKA MOJAWAPO YA KITUO WILAYANI IKUNGI (IGLANSONI)



- QTY issued to dispensing area FOR the last 3months including IPD
- QTY dispensed in the last 3months (As indicated in Dispensing register)
- Stock available at the dispensing area at the day of audit
- Preferage

Nini Kifanyike.....


1. Wafamasia wa Wilaya kufanya majukumu yao kwa kuhakikisha bidhaa zote muhimu za afya zinakuwepo vituoni wakati wote.
2. Kufanya mafunzo kwa watumishi wapya walioajiriwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuondoa changamoto katika usimamizi wa dawa na vifaa tiba.
3. Kufanya usimamizi shirikishi wenye tija kwa kubaini changamoto mbalimbali na kuainisha njia za kuzikabili.
4. Kila Watendaji wa Halmashauri kuhakikisha kumbukumbu za matumizi na utunzaji wa dawa zinawekwa vizuri wakati wote.
5. Kila kituo kutumia vitendea kazi vyote vinavyohitajika katika utoaji huduma kwa wateja/wagonjwa.
6. Kufanya uhakiki wa mara kwa mara wa matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba katika ngazi ya vituo.

Nini kifanyike.....

7. Mfamasia wa Wilaya kuhakikisha anafanya mgawanyo wa dawa katika vituo kuzuia Mrundikano wa dawa katika baadhi ya vituo na kuhakikisha upatikanaji wa dawa wakati wote katika vituo.
8. Kuimarisha mawasiliano baina ya wataalamu wa dawa walioko wilayani na Mfamasia ngazi ya Mkoa ili kupunguza changamoto za kitaalamu zinazojitokeza.
9. Kufanya usimamizi na ukaguzi katika vituo binafsi (Maduka ya dawa) na kuhakikisha vinafanya kazi kwa kufuata taratibu na miongozo iliyopo.
10. Kuwachukulia hatua watumishi wote wataoonekana kutumia vibaya mali za umma kwa manufaa binafsi.
11. Kuwachukulia hatua watumishi wanaokaidi kutumia vitendea kazi na kusababisha Upotevu usiokuwa wa lazima wa dawa na vifaa tiba.



Tathmini ya awali katika vituo vya kutolea huduma za Afya Feb.2016 N=5326



Matokeo ya Tathmini ya uandaaji wa mipango ya Halmashauri (CCHP-2016/17)

6.6 Regional Performance Scores

Name of region	Performance Score (%)
1. Singida Region	100
2. Arusha Region	89
3. Katavi Region	87
4. Iringa Region	87
5. Njombe Region	87
6. Mbeya Region	82
7. Tabora Region	77
8. Dodoma Region	76
9. Rukwa Region	75
10. Manyara Region	72
11. Simiyu Region	63
12. Kilimanjaro Region	61
13. Morogoro Region	59
14. Kagera Region	56

15. Mara Region	53
16. Ruvuma Region	50
17. Tanga Region	47
18. Lindi Region	40
19. Kigoma Region	35
20. Mwanza Region	26
21. Mtwara Region	25
22. Shinyanga Region	22
23. Dar Es Salaam Region	0
24. Geita Region	0
25. Pwani Region	0

1.5 MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

- Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) umeanzishwa kwa madhumuni ya kuwapunguzia gharama za matibabu Wananchi kwa kuwawezesha kuchangia gharama nafuu kwa kaya au kikundi na kupata kadi ya matibabu ya kipindi cha mwaka mmoja.




Mkoa wa Singida ni miiongoni mwa Mikoa ambayo Wananchi wake wameitikia vizuri kujiunga na mfuko huu japo kuna kaya chache zilizojiunga


Halmashauri nyingine kutoka Mikoa mbalimbali zimeendelea kuja Singida kujifunza jinsi ya kuendesha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

Mwongozo wa matumizi ya fedha za CHF

Shughuli	Asilimia
Dawa	67%
Vifaa tiba	15%
Elimu ya Uhamasishaji	10%
Posho ya Wakusanyaji	5%
Mengineyo	3%




Kaya zilizotarajiwa Vs zilizojiunga mwaka 2015



Wastani wa Mkoa ni kaya 60,899

Kaya zilizotarajiwa Vs kaya zilizojiunga (Jan – Aug 2016)



Taarifa ya Fedha za mfuko wa Afya ya Jamii 2014, 2015 na Januari hadi Machi 2016

Jina la Halimashauri	Kiasi cha fedha kilichokusanya	Kiasi cha fedha za Tele kwa Tele zilizopokelewa	Jumla fedha zilizokusanywa
Singida MC	56,637,000	22,309,000	78,946,000
Singida DC	152,840,000	154,700,000	307,540,000
Iramba DC	227,579,000	291,090,000	518,669,000
Manyoni DC	173,044,000	89,360,000	262,404,000
Ikungi DC	171,810,000	282,130,000	453,940,000
Mkalama DC	254,465,000	-	254,465,000
Itigi DC	8,390,000	-	8,390,000
Jumla	1,044,765,000	839,589,000	1,884,354,000

Taarifa ya Fedha za mfuko wa Afya ya Jamii

Januari hadi Agosti, 2016


Jina la Halimashauri	Kiasi cha fedha kilichokusanya	Kiasi cha fedha za Tele kwa Tele zilizopokelewa	Jumla fedha zilizokusanywa
Singida MC	26,805,000	0	26,805,000
Singida DC	42,480,000	32,500,000	74,980,000
Iramba DC	78,040,000	151,400,000	229,440,000
Manyoni DC	58,520,000	40,215,000	98,735,000
Ikungi DC	72,980,000	0	72,980,000
Mkalama DC	34951	34,220,000	34,254,951
Itigi DC	0	0	0
Jumla	278,859,951	258,335,000	537,194,951

Changamoto Zinazokabili eneo la Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

- ▶ Baadhi ya Halmashauri kutozingatia miongozo ya matumizi ya fedha za CHF kama ilivyotajwa hapo awali.
- ▶ Baadhi ya vijiji kutokuwa na vituo vya kutolea huduma za Afya .
- ▶ Baadhi ya huduma kama za Maabara kukosekana katika Zahanati hivyo kuchangia wananchi wengi kushindwa kujiunga na CHF.
- ▶ Hakuna mfumo mzuri wa rufaa za wagonjwa wanaotumia CHF kutoka katika ngazi ya Zahanati na Vituo vya Afya kwenda ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.
- ▶ Mkoa unashauri utaratibu wa rufaa ya wateja wa CHF ndani ya wilaya na mkoa uanze kutumika.

HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA MTOTO

- Kati ya vituo 221, ni vituo 203 sawa na 92% vinatoa huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto;
- 89% vinatoa huduma za Uzazi wa Mpango,
- 90% huduma za Wazazi,
- 90% huduma za kumsaidia mtoto kupumua,
- 95% huduma za matibabu ya watoto kwa uwiano,
- 96% huduma za chanjo,
- 92% huduma za PMTCT,
- 96% huduma za chanjo,
- 0% huduma ya Upasuaji na Damu salama ngazi ya (vituo vya Afya - 17)



Kiwango cha upimaji wa VVU kwa akina mama wajawazito- 2014,2015,Jan- Agosti-2016

	2014	2015	Jan – Agosti 2016
Idaddi ya Wajawazito hudhurio la kwanza	68,266	67,747	31986
Idadi ya wajawazito waliopima VVU katika hudhurio la kwanza	56,757	56,947	27968
Asilimia ya wajawazito waliopima VVU katika hudhurio la kwanza	83%	84%	87%

Huduma za wazazi-waliotarajiwa, jumla ya waliojifungua, waliojifungulia vituoni na asilimia ya-2014,2015,Jan-Agosti-2016

	2014	2015	Jan-Agosti,2016
Wazazi waliotarajiwa	47,837	50,627	34537
Jumla ya waliojifungua	46,146	45,348	29072
Waliojifungulia katika vituo vya kutolea huduma	38,609	41,548	27108
% ya waliojifungulia vituoni	81%	82%	78%

Halmashau ri	2014		2015		2016 (Jan - Sept 2016)	
	Vizazi hai	Idadi ya vifo	Vizazi Hai	Idadi ya vifo	Vizazi Hai	Idadi ya vifo
Ikungi	7,280	8	7,602	16	5852	5
Iramba	6,520	8	6,982	7	4501	6
Manyoni	10,729	14	10,640	13	4356	4
Itigi	-	-	-	-	2081	6
Mkalama	3,856	2	5,122	4	3888	2
Singida DC	4,711	3	3,931	1	2222	1
Singida MC	8,303	19	9,434	19	5880	9
Mkoa	41,399	54	43,711	60	28780	33
MMR		130/10000		137/1000		27=94/100,00

Vifo vyatiafia kwa sasa ni 432/100,000
 vazazi hai. na ifikapo 2020 tunatakiwa kufikia 292/100,000.Wakati katika kipindi
 cha Jan hadi Septemba kuna vifo ni 33,Ratio ya 94/100,000 ni Jan-Agosti
 hapa kuna vifo 27=94/100,000.

Sababu za vifo vya wazazi

Jan-Sept 2016

	Jamii	Kituoni
Kutoka damu (PPH)	6	6
Kifafa cha Mimba	0	4
Kuchanika kizazi	1	4
Embolism	0	3
Uambukizo	0	2
Madhara ya dawa za usingizi	0	1
Upungufu wa damu	0	3
Magonjwa ya moyo	0	2
Kuachia kwa kondo la nyuma(Abruptio placenta)	0	1
Jumla	7 (21%)	26 (79%)

Idadi ya vifo vya watoto siku 0-28 Chini ya mwaka 1 na chini ya miaka 5 Jan-Agost 2016

Wilaya	0-28	Chini ya mwaka 1	Chini ya miaka 5	Vizazi hai
Ikungi	23	35	66	5852
Iramba	14	31	56	4501
Itigi	20	37	70	2081
Manyoni	5	27	53	4356
Mkalama	14	20	28	3888
Singida DC	14	25	34	2222
Singida MC	62	93	127	5880
Mkoa	152	268	431	28780
Uwiano-Mkoa	5/1000	9/1000	15/1000	-

Changamoto


- Ni vituo 2 vya afya kati ya 17 vimefikia vigezo vya kutoa huduma za BEmONC
- Hakuna Zahanati hata moja yenye uwezo wa hutoa huduma za BEmONC
- Hakuna kituo cha Afya hata kimoja kinachotoa huduma za dharura kwa wazazi(CEmONC)
- Bado kuna baadhi ya vituo havitoi huduma za afya ya uzazi na mtoto

Changamoto.....

- Ushiriki mdogo wa wanaume kwenye maswala ya afya ya uzazi
- Ukusanyaji na utunzaji wa takwimu bado ni tatizo toka kwenye vyanzo mbalimbali,mfano Regista ,Muoanisho na taarifa ya mwezi takwimu kutokuoana
- Ni hospitali 2 tu kati ya 9 hutoa huduma za KMC

HUDUMA ZA CHANJO

Mkoa wa Singida una jumla ya vituo **221** vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo, vituo **192** vinatoa huduma za chanjo kwa mama wajawazito na watoto, hii ikiwa ni **asilimia 87** ya vituo vyote .



HUDUMA ZINAZOTOLEWA

Huduma za chanjo Zinazotolewa zimegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni;

- Utoaji wa chanjo mbalimbali kwa walengwa ambao ni watoto chini ya umri wa **miaka 5** na akina mama wajawazito.
- Utunzaji wa mnyororo baridi ili kuhakikisha kuwa chanjo zinazotolewa kwa walengwa wote zinabaki katika ubora uleule kuanzia kiwandani hadi kwa mtumiaji.
- Ufutiliaji wa taarifa za magonjwa yanayozuulika kwa chanjo ili kupima mafanikio ya huduma zinazotolewa

Chanjo Zinazotolewa

Kwa sasa kuna aina 7 za chanjo zinazotolewa nchini,

- 6; kati ya hizo zikiwa ni maalum kwa ajili ya watoto chini ya miaka 5(DTP, Polio, Surua-Rubella, PCV, BCG chanjo dhidi ya Rotavirus)
- 1; ni chanjo inatotolewa kwa ajili ya akina mama wajawazito ili kumkinga mama na mtoto dhidi ya ugonjwa wa Pepopunda.



Hali ya Uchanjaji kwa Mwaka 2015 (Walengwa 50,627)

Antigen	Dozi ya Kwanza	Dozi ya Mwisho	Kiwango cha Uasi
DTP (Penta)	64,467 (126%)	56,434 (111%)	15%
OPV	62,838 (123%)	55,320 (109%)	14%
Measles-Rubella	57,855 (114%)	27,919 (60%)	40%
Rotavirus	65,533 (128%)	58,982 (116%)	12%
PCV13	64,409 (125%)	56,823 (112%)	13%
BCG	96,461 (192%)	-	-
Pepopunda	33,025 (66%)	48,387 (94%)	-

Hali ya Uchanjaji Jan-Aug 2016 (Walengwa 51,817)

Chanjo	Dozi ya Kwanza	Dozi ya Mwisho	Kawango cha Uasi
DTP (Penta)	42,955 (83%)	41,053 (79%)	4%
OPV	42,152 (81%)	40,282 (78%)	4%
Measles-Rubella	39,078 (75%)	33,702 (65%)	14%
Rotavirus	43,430 (84%)	41,287 (80%)	5%
PCV13	43,171 (83%)	41,141 (79%)	5%
BCG	63,047 (122%)	-	
TT	23,120 (45%)	35,380(68%)	

Utendaji Kwa Halmashauri

Halmashauri	DTP3 2015 (%)	DTP3 Jan-Aug 2016(%)
IKUNGI	119	86
IRAMBA	113	82
MANYONI	107	90
MKALAMA	94	60
SINDIGA DC	117	75
SINGIDA MC	117	76

Changamoto

- ▶ Baadhi ya vituo kutokutoa huduma za chanjo kwa kukosa majokofu (Jokofu moja ni dola 3,000, hivyo halamshauri zinapaswa kusaidia Wizara katika ununuzi kwa kutumia vyanzo vyake)
- ▶ Ukosefu wa umeme mbadala kwa baadhi ya halamshauri (Singida DC, Singida MC, Ikungi). Halmashauri hizi zinahataraisha usalama wa chanjo wanazotunza zinazokadiriwa kufikia THS 500mil kwa kila robo mwaka.
- ▶ Upungufu wa mitungi ya gesi kwenye vituo na halmashauri kutokufanya manunuzi kwa wakati na kusababisha huduma kufungwa hivyo kusitisha huduma mara kwa mara
- ▶ Halmashauri kutokuwa na usimamizi mzuri wa huduma za chanjo (Mkalama) kwa kuzingatia taarifa za utendaji
- ▶ Matumizi mabaya ya magari ya chanjo na kusababisha usambazaji wa chanjo kwenye vituo kutokufuata ratiba

Vituo Ambavyo Havitoi Huduma za Chanjo

WILAYA	VITUO AMBAVYO HAVITOI CHANJO KWA KUKOSA JOKOFU
Ikungi =3	Mungaa, Makotea, Makilawa
Iramba = 3	Ushora Magereza, Kinampanda TTC, Bomani Magereza
Manyoni =11	Lusilile, Magereza, Kalangali, Riziki Maternity Home, Chitinde, HekaAzimio, Kitalalo, Mvumi, Makale, Kintanula, Doroto
Mkalama = 2	Mgimba, Samaria
Singida DC = 5	Mjughuda, Mkenge, Iamba, Itamka, Kijota

USTAWI WA JAMII

Shughuli kuu ya Ustawi wa Jamii katika Mkoa ni kuhakikisha kuwa Jamii ya wanasingida inaishi kwa kuzingatia haki, usawa, ustawi na maendeleo kwa makundi yote.

Shughuli zilizotekelizwa mwaka 2015

Halmashauri	Mashauri ya Ndoa	Matunzo	Mimba/Watoto nje ya ndoa	Jumla
Sigida MC	317	52	94	463
Manyoni	219	36	59	314
Ikungi	118	67	73	258
Singida DC	78	43	39	160
Iramba	112	74	91	277
Mkalama	44	38	51	113
Jumla Kimkoa	888	310	407	1,605

Ukatili wa Kijinsia na Ukatili dhidi ya Watoto

Aina ya Ukatili wa kijinsia/Watoto	Miaka 0 - 18		Jumla	Miaka 18+		Jumla
	Me	Ke		Me	Ke	
Kupigwa	54	84	138	12	66	78
Kubakwa	0	14	14	0	6	6
Kulawitiwa	30	12	42	2	0	2
Ngono kinyume na Maumbile	6	21	27	7	18	25
Kunyimwa Mahitaji muhimu	110	124	234	18	90	108
Kutelekezwa	19	17	36	6	10	16
Kutelekeza watoto	0	6	6	19	8	27
Kutupa watoto	0	8	8	0	0	0
JUMLA	219	286	505	64	198	262⁴

Mashauri yaliyopokelewa kwa mwaka 2015

Na	Aina ya shauri	Idadi ya yaliyopokelewa
1	Ndoa	888
2	Nje ya ndoa	407
3	Matunzo ya watoto	310
4	Ukatili wa kijinsia	262
5	Ukatili dhidi ya watoto	505
	Jumla	2372

Mashauri yaliyopokelewa Mwezi

Januari - Agosti 2016

Na	Aina ya Shauri	Idadi ya yaliyopokelewa
1	Ndoa	442
2	Nje ya ndoa	268
3	Matunzo ya watoto	357
4	Ukatili wa kijinsia	65
5	Ukatili dhidi ya Watoto	104
Jumla		1236

Watoto walio katika Mkinzano na Sheria

Kwa kipindi cha Januari hadi Agosti Jumla ya watoto 31 wamekuwa kwenye mkinzano na sheria kwa kufanya makosa mbalimbali ikiwa pamoja na,

- ✓ Kuua - 3
- ✓ Kubaka - 4
- ✓ Kulawiti - 14
- ✓ Kujeruhi - 3
- ✓ Wizi – 2
- ✓ Ushahidi Mahakamani - 5

Kilichofanyika ili kupunguza Matukio

Elimu mbalimbali zilizotolewa kwa kipindi cha Januari hadi Agosti 2016 na idadi ya watu walio pata elimu hizo

- Malezi bora kwa watoto kwa watu - 255
- Ulinzi na usalama wa mtoto kwa watu - 586
- Ukatili wa kijinsia kwa watu - 27

Changamoto

- ❑ Ongezeko kubwa la watoto walio katika mazingira hatarishi hasa wa mitaani kwani kwa mwaka 2014/15 jumla ya watoto 36,246 Waligundulika wapo katika mazingira hatarishi.
- ❑ Kuwepo kwa vituo/ makao machache ya watoto walio katika mazingira hatarishi kwani hivi sasa mkoa wa Singida una jumla ya makao 4 tu yenye jumla ya watoto 90 ambayo ni idadi ndogo sana ukilinganisha na watoto wanaohitaji huduma hiyo.
- ❑ Kutokuwepo kwa one stop centre kwa ajili ya wahanga mbalimbali wa matukio ya ukatili.
- ❑ Ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto .
- ❑ Kutokuwepo kwa Timu za Ulinzi wa Mtoto kuanzia ngazi ya Halmashauri hadi Kata hivyo kusababisha matatizo mengi ya watoto kushindwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

HALI YA MAAMBUKIZI YA VVU NA UKIMWI NA HUDUMA ZA CTC

- Kiwango cha maambukizi ya UKIMWI katika Mkoa kinaendelea kupungua kila mwaka mfano mwaka 2014 prevalence rate ilikuwa 3.4% Na mwaka 2015 (3.1%)

Halmashauri	Waliopima 2014	Waliokutwa na maambukizi 2014	HIV Prevalence %	Waliopimwa 2015	Waliokutwa na maambukizi 2015	HIV Prevalence %
Iramba	25,927	1,307	5.0	23,683	823	3.5
Manyoni	34,261	1,407	4.1	31,862	1,227	3.9
Singida MC	23,988	920	3.8	26,513	1,301	4.9
Singida DC	15,945	144	0.9	20,684	222	1.1
Ikungi	16,639	453	2.7	19,950	401	2.0
Mkalama	11,051	122	1.1	12,504	181	1.4
Mkoa	127,811	4,353	3.4	135,196	4,155	3.1

HUDUMA ZA MATUNZO NA TIBA KWA WATU WANAOISHI NA VVU

- Huduma za matibabu kwa wagonjwa wenyewe maambukizi ya VVU zinatolewa katika vituo 34 ndani ya Mkoa kati ya vituo vya kutolea huduma 221. Kuna jumla**

Halmashauri	Hospitali	Vituo vya Afya	zahanati	Jumla
Iramba	1	2	1	4
Manyoni	3	3	4	10
Singida MC	1	1	2	4
Singida DC	1	2	2	5
Ikungi	2	3	2	7
Mkalama	1	2	1	4
Jumla	9	13	12	34

Idadi ya wagonjwa waliosajiliwa na kuanzishiwa dawa katika kiliniki za matunzo na tiba

Halmashauri	Mwaka 2014		Mwaka 2015		Jan-March 2016	
	Waliosajiliwa	Wanaopata dawa	waliosajiliwa	Wanaopata dawa	Waliosajiliwa	Wanaopata dawa
Iramba	4,765	1,869	6,154	2,505	5,543	2,383
Manyoni	4,832	2,133	5,631	2,541	3,506	1,607
Singida MC	6,260	1,943	7,039	2,256	7,273	2,460
Singida DC	584	261	889	403	783	384
Ikungi	1,716	777	1,863	836	2,181	325
Mkalama	1,339	645	601	392	1,550	895
Itigi DC	NA	NA	NA	NA	2,338	1,132
JUMLA	19,496	7,628	22,177	8,933	23,174	9,186

Idadi ya watoto wa chini ya miaka 15 waliosajiliwa katika kiliniki za matunzo na tiba na kuanzishiwa dawa

Halmashauri	Mwaka 2014		Mwaka 2015		January hadi Machi 2016			
	Waliosajiliwa	Wanaopata dawa	Waliosajiliwa	Wanaopata dawa	Waliosajiliwa	Wanaopata dawa	<5	5-15
Iramba	437	127	444	170	196	301	24	133
Manyoni	367	141	434	185	103	161	25	83
Singida MC	460	206	514	152	226	294	26	130
Singida DC	68	25	73	49	46	37	7	32
Ikungi	151	49	160	21	88	94	13	70
Mkalama	92	31	55	25	61	72	27	37
Itigi DC	0	0	0	0	89	96	18	72
JUMLA	1,575	579	1,680	602	809	1055	140	557

CHANGAMOTO

- Upungufu wa kiliniki za matunzo na tiba kwa asilimia 85%
- Mila na desturi potofu
- Mabadiliko ya tabia (Behaviour change)
- Huduma za wagonjwa wa UKIMWI majumbani bado ni hafifu kutoka na kuwa na watumishi wachache na vitendea kazi vichache kuwafikia majumbani mwao kuwashudumia.
- Wagonjwa wengi kuacha kuhuduria katika vituo vyatunzo namatibabu ya UKIMWI (lost to follow up).

HALI YA LISHE YA MKOA

- Kutokana na utafiti wa Afya ya mama na mtoto (TDHS, 2015) ilionekana:-
 - ❑ **34.5%** ya watoto chini ya miaka 5 wana udumavu, **5%** wana ukondefu ,**12%** wana uzito pungufu.
 - ❑ **36%** ya watoto chini ya miaka mitano wana Upungufu wa damu (Anemia).
 - ❑ **26%** ya wanawake(15-49 miaka) wana upungufu wa damu (Anemia).
- Wadau wanaosaidia masuala ya lishe katika mkoa ni World vision, PANITA, Pamoja Tuwalee, Helvetas, WFP n.k

UZITO PUNGUFU

- ❑ Uzito pungufu ni moja ya viashiria vya utapiamlo, huweza sababishwa na ulaji duni na magonjwa.
- ❑ Lishe ya mama kabla na wakati wa ujauzito huathiri uzito wa kuzaliwa wa mtoto.
- ❑ Uzito pungufu kwa watoto huongeza uwezekano wa mtoto kupata magonjwa mf. Kuhara , nimonia n.k.

UZITO PUNGUFU - KLINIKI YA WATOTO



HALMASHAURI	WATOTO WALIOPIM A UZITO (2015)	WATOTO WALIOKUWA NA UTAPIAMLO.	ASILIMIA YA WATOTO WALIOKUWA NA UTAPIAMLO	WATOTO WALIOPIMA UZITO (2016)	WATOTO WALIO NA UZITO PUNGUFU (2016) .	ASILIMIA UTAPIAMLO (2016)
	150903	12,267	8%	107104	2561	2%
SINGIDA DC	119469	11,861	9%	95724	5101	5%
MANYONI DC	139042	20,482	13%	32889	6102	19%
MKALAMA DC	116486	11776	9%	82032	2747	3%
IRAMBA DC	175052	8,606	5%	131006	4939	4%
SINGIDA MC	96404	5143	5%	73059	3108	4%
ITIGI DC				44853	1077	2%
REGION (TOTAL)	666,667	70,135	8%	566667	25635	5%

UZITO MKUBWA

- Uzito uliokithiri ni moja ya aina ya utapiamlo.
- Uzito wa Mwili hutegemea kiasi , aina ya chakula unachokula pamoja na shughuli unazofanya.
- Unene uliokithiri unachangia kwa kiwango kikubwa kupata magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, magonjwa ya moyo n.k


HALI YA LISHE - WAJUMBE KIKAO CHA WADAU.

WALIOPIMA 93



- % UZITO ULIOZIDI
- % UZITO MKUBWA SANA
- % HALI NZURI

Magonjwa sugu yasiyoambukiza (2014& 2015)



ATHARI ZA UTAPIAMLO


- Kupungua kwa uwezo wa akili hivyo watoto kupata ugumu wa kufundishika na kuelewa.
- Kuchelewa katika hatua za ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili.
- Kuongezeka kwa magonjwa na vifo vya watoto.
- Kuongezeka kwa magonjwa na vifo kwa wanawake wajawazito.
- Kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi na uzalishaji mali.
- Kuongezeka kwa magonjwa na vifo vitokanavyo na magonjwa sugu yasiyoyakuambukiza.

Athari ya Udu^mavu katika ukuaji wa ubongo

kawaida



Dumavu



Typical brain cells

Extensive branching

Impaired brain cells

Limited branching

Abnormal, shorter branches

CHANGAMOTO

- Ukosefu wa vifaa vya kufanyia tathimini ya hali ya Lishe.
- Kamati za lishe hazikai vikao vya kila robo mwaka. Wenyekiti wa kamati hizo ni RAS/DED, Katibu ni Afisa Lishe na wajumbe ni wakuu wa Idara (Afya, Mipango, Kilimo, uvuvi na Mifugo, maendeleo ya jamii, Maji na elimu).
- Uchache wa wataalamu wa Lishe katika mkoa.
- Kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi na uzalishaji mali.
- Kuongezeka kwa magonjwa na vifo vitokanavyo na magonjwa sugu yasiyoyakuambukiza.

Hali ya upatikanaji wa vyoo,

Juni, 2016

S/N	JINA LA HALMASHAURI	IDADI YA KAYA	IDADI YA VYOO BORA	%	IDADI YA VYOO VYA MUDA/ASILI	%	IDADI YA KAYA ZISIZOKUWA NA VYOO	%	Kunawa mikono nje ya choo	%
1	SINGIDA DC	34241	7577	22.1	21635	63.2	5029	14.7	6570	16
2	SINGIDA MC	32389	20623	63.7	11336	35.0	430	1.3	508	2
3	IRAMBA	50431	15863	31.5	27953	55.4	6615	13.1	11389	22
4	MKALAMA	34966	12000	34.3	20417	58.4	2549	7.3	367	1
5	ITIGI	22701	2275	10.0	9123	40.2	11303	49.8	175	0.7
6	MANYONI	39022	5765	14.8	14173	36.3	19084	48.9	469	1
7	IKUNGI	55829	11280	20.2	40187	72.0	4411	7.9	1479	3
	JUMLA	269579	75383	28.0	144824	53.7	49421	18.3	20957	7.8

Athari za kutokujenga na kutumia vyoo

- Kuchafuliwa kwa vyanzo vya maji na vyakula
- Kuenea kwa magonjwa mbalimbali katika jamii hasa ya kuhara
- Kuongezeka kwa wagonjwa wa kuhara kutoka 80,274 (2010) hadi 119,837 (2015)
- Kuleta umaskini kutokana na wananchi kuugua mara kwa mara
- Huchangia vifo vitokanavyo na magonjwa kuhara

Changamoto

- Baadhi ya kaya kutokujenga na kutumia vyoo ambapo 18.3% ya kaya hazina vyoo
- Uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi juu ya umuhimu wa kujenga na kutumia choo
- Baadhi ya Wananchi kujisaidia hovyo na kuchafua mazingira

Mikakati ya Mkoa


- Mkoa ushaziagiza halmashauri zote tangu 27 Mei, 2016 kusimamia sheria za afya mazingira na kuhakikisha kila kaya inajenga na kutumia choo
- Kushirikiana na halmashauri Kutoa elimu ya afya kwa wananchi hasa ujenzi wa vyoo na unawaji mikono.

Damu salama

Makundi maalum yanayohitaji damu ni kama yafuatayo:

- Mama wajawazito wanaohitaji upasuaji
- Watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) ambao seli zao zinakuwa hazijakamilika kutokana na ukosefu wa virutubisho,
- Watoto wenyewe matatizo ya ugonjwa wa selimundu (sickle cell)
- Waathirika wa Ajali mbalimbali
- Wagonjwa wengine wanaohitaji upasuaji mkubwa


MAKUSANYO YA DAMU KATIKA MKOA WA SINGIDA KUANZIA Januari – Sept, 2016.



**KIASI CHA DAMU KILICHOKUSANYWA NA MATOKEO YA
VIPIMO – JAN –SEPT 2016**

MIEZI	Kiasi cha damu iliyokusany wa na kupimwa	HIV	HB V	HC V	SYPHIL IS	TOTA L
JAN 2016	157	4	11	4	6	25
FEB 2016	256	0	17	4	0	21
MAR 2016	164	2	5	4	4	15
APRL 2016	349	2	21	4	6	33
MAY	0	0	0	0	0	0
JUNE	0	0	0	0	0	0
JULY-SEPT	692	22	25	13	17	77
TOTAL						

MGAWANYO YA DAMU KATIKA MKOA WA SINGIDA JAN-SEPT 2016



Changamoto zinazoikabili Timu ya ukusanyaji damu ni kama hifuatavyo:

- Vitendeakazi havitoshelezi
- Ukosefu wa Fedha za kuendeshea shughuli nzima za ukusanyaji wa damu, (viburudisho kwa wachangiaji damu) na dharura nyinginezo zinazojitokeza wakati wa Zoezi la uchangiaji damu na baada ya zoezi.
- Hamasa kwa Jamii juu ya suala zima la uchangiaji Damu.
- Uuzaji wa damu kwa Watumishi wa Afya wasio waadilifu na ndugu wa Wagonjwa kununua Watu wa kutoa damu

HUDUMA/KLINIKI TEMBEZI KATIKA MKOA WA SINGIDA

- Katika kukabiliana na uhitaji mkubwa wa huduma za kibingwa kwa wagonjwa waliopo Mkoani humu, uongozi wa Mkoa ulianzisha huduma za kibingwa kwa kutumia wataalamu waliopo Mkoani na kualika wachache kutoka nje ya mkoa ili kuwahudumia wagonjwa ambao wangehitaji huduma hizi nje ya mkoa na isitoshe kwa gharama za juu.
- Huduma hizi tembezi zimezinduliwa rasmi mwezi August 2016 katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na inaendelea katika Halmashauri nyingine ambapo sasa huduma zinatolewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika hospitali ya Mtinko kuanzia tarehe 26/9/2016 – 30/9/2016.

Huduma za kibingwa.....Wagonjwa waliohudumiwa Wilayani Iramba

- Jumla ya wagonjwa 1357 walionwa.

S/N	ENEO/IDARA	IDADI YA WAGONJWA WALIOONWA
1	MENO	141
2	WATOTO	104
3	WANAWAKE	164
4	UPASUAJI	160
5	MAGONJWA YA NDANI	262
6	MACHO	341
7	UJUMLA (GENERAL)	185
	JUMLA	1357

MENO

S/N	MATIBABU	IDADI YA WAGONJWA
1	Kung'olewa	65
2	kuzibwa	33
3	Kusafisha meno	33
4	Upasuaji mdogo wa Ulimi	5
5	Kuunganisha meno	3
6	Rufaa	2

S/N	AINA YA UGONJWA	IDADI
1	Mtindio wa Ubongo	13
2	Magonjwa ya njia ya Hewa	19
3	Selimundu (SCD)	8
4	Fangasi za Ngozi	9
5	Kifafa	6
6	Kifua Kikuu cha mifupa	2
7	Uvimbe	2
8	Matundu kwenye moyo	2
9	Mengineyo	40
10	Rufaa	3

UPASUAJI

S/N	Aina ya Ugonjwa	Aina ya upasuaji uliofanyika	Idadi
1	Ngili kavu ya kitovu kwa watoto	Herniorraphy	6
2	Ngili kavu waliyozaliwa nayo watoto	Herniotomy	5
3	Ngili kavu na ya maji kwa wakubwa	Herniorraphy/Hydrocelectomy	10
4	Goita	Thyroidectomy	1
5	Tezi Dume	Prostatectomy	1
6	Kuziba kwanjia ya haja ndogo(me)	Suprapubic catheterization	1
7	Kuvimba kwa tezi za koo	Tonsilectomy	3
8	Ngili ya chembe	Herniorraphy	3
9	Nyinginezo	Ecission/contracture release	3

Huduma tembezi za kibingwa.....

- Wagonjwa wenyе mahitaji ya huduma zakibingwa wameongezeka katika Hospitali zetu
- Imeonekana kuna haja ya kutenga muda wa kutosha na rasilimali fedha kwa ajili ya huduma hizi katika Halmashauri zetu.
- Shukrani za dhati zinatolewa kwa timu ya usimamizi wa afya ya Wilaya na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa ujumla.